## CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

## TAASISI YA TAALUMA ZA KISWAHILI

## IDARA YA FASIHI, MAWASILIANO NA UCHAPISHAJI

**JINA LA KOZI:** USHAIRI WA KISWAHILI

**MSIMBO WA KOZI:** KF 223

**JINA LA MSIMAMIZI:** DKT. HAFIDHA MHANDO

**SIKU YA SEMINA:** JUMATATU

**MUDA:** SAA 7:00 – 8:00 ASUBUHI

**CHUMBA:** ALRB

**AINA YA KAZI:** KAZI YA KIKUNDI

**TAREHE YA KUWASILISHA:** 11/12/2023

### MAJINA YA WASHIRIKI

| NA. | JINA LA MWANAFUNZI | NAMBA YA USAJILI | PROGRAMU | SAINI |
|---|---|---|---|---|
| 01 | SAIGODI FAITH DICKSON | 2022-04-11717 | BAED | |
| 02 | SAMWEL HAPPINES JOHN | 2022-04-11879 | BAK | |
| 03 | MKASANGA WINIFRIDA CHARLES | 2022-04-07617 | BAED | |
| 04 | THOMAS NEEMA JISENA | 2022-04-12994 | BAED | |
| 05 | NGOWI EMMANUEL HENDRY | 2022-04-10324 | BAK | |
| 06 | MICHAEL IRENE JOSHUA | 2022-04-07425 | BAED | |
| 07 | MATHIAS BERTHA ROBERT | 2022-04-06649 | BAED | |
| 08 | GWANGINEZA ABAS WILLIAM | 2022-04-02189 | BAED | |
| 09 | HASHIMU RAMADHANI MOHAMED | 2022-04-08101 | BAED | |
| 10 | EMANUEL ENATHA NYEGORO | 2022-04-01743 | BAED | |

www.dyampaye.co.tz

## SWALI LA 04

Chambua mitindo ya mashairi katika diwani ya *Tuzo ya Ebrahimu Hussein (Toleo la III)*. Mitindo hiyo ina dhima gani katika utunzi wa mashairi ya Kiswahili.

Kazi hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu. Sehemu ya kwanza ni utangulizi ambapo, imefafanuliwa dhana ya mtindo kwa kurejelea wataalamu kadha wa kadha. Sehemu ya pili ni kiini ambapo mitindo mbalimbali ya mashairi imeelezewa kama ilivyojitokeza katika diwani ya *Tuzo za Ebrahim Hussein (Toleo la Tatu*). Aidha, katika sehemu ya tatu ambayo ni hitimisho, yametolewa maoni kwa watunzi wa mashairi katika utumiaji wa mitindo hiyo.

Senkoro (1982) anasema mtindo katika kazi ya fasihi ni ile namna ambayo msanii hutunga kazi hiyo na kuipa sura ambayo kifani na kimaudhui huainisha kanuni au kawaida zilizofuatwa (za kimapokeo) ama ni za kipekee. Senkoro anatueleza kwamba mtindo huhusisha upangaji wa fani na maudhui katika kazi ya fasihi ambapo upangaji huu hutegemea upekee alionao msanii, kwa maana kwamba jambo moja linaweza kuongelewa na wasanii wawili tofauti lakini namna linavyowasilishwa likatofautiana, na hii ni kulingana na upekee wao. Kwa mujibu wa Wamitila (2003) mtindo ni ule upekee alionao mtunzi wa kazi ya kifasihi katika kuipa kazi yake sura fulani, kifani na kimaudhui. Anaendelea kusema, dhana ya mtindo hurejelea sifa maalumu za mwandishi au mazoea ya mwandishi fulani ambayo hujionyesha kwenye fani yake. Wamitila anaenda mbali zaidi, kuwa upekee huo unaweza kubainishwa baada ya kupitia kazi kadhaa za mtunzi. Kwa ujumla mtindo ni ule upekee alionao mtunzi wa kazi ya fasihi katika kuipa kazi zake sura fulani kifani na kimaudhui unaomtofautisha yeye na mtunzi mwingine hata kama kitu kinachoongelewa ni kilekile. Katika utunzi wa mashairi, watunzi hutumia mitindo kadha wa kadha, kwa kurejelea diwani ya *Tuzo ya Ebrahim Hussein* (Toleo la III: 2014-2020) ifuatayo ni mitindo ya mashairi iliyojidhihirisha katika diwani hii;

Mtindo wa pindu, Mulokozi (2017) anaeleza neno "pindu" katika ushairi lina maana mbili. Mosi, ni mbinu ya kulifanya neno au sehemu ya neno la mwisho la kipande au mstari lirudiwe mwanzoni mwa kipande au mshororo unaofuata. Pili ni kugeuza silabi za mwanzo za neno zikaja mwisho, kwa mfano "kata" kuwa "taka". Utofauti kati ya mtindo wa pindu na kikufu, ni kwamba pindu huhusisha neno lakini kikufu huusisha kipande. Katika diwani ya *Tuzo ya Ebrahim Hussein* mtindo huu umedhihirika kwenye shairi la *Mateka Tumetekeka* ukurasa wa 240, mfano ubeti wa kwanza anasema;

"Awali wangu **utungo**, **utungo** nauandika,
Naandika penye **pengo**, **pengo** lipate zibika…"

www.dyampaye.co.tz


Mwandishi ameyafaya maneno yaliyokozwa ya mwisho katika ukwapi yawe ya mwanzo katika utao.

Mtindo wa kidatu, kwa mujibu wa TET (2019), katika kidatu baadhi ya mistari hufupishwa maneno yake au silabi zake tofauti na mistari mingine ambayo huwa na silabi au maneno mengi. Kwa msingi wa dhana hii, kwa mfano shairi lina mizani ya jumla ya 18 kwa kila mshororo mmoja, basi mshororo mmoja au zaidi katika huo ubeti huwa na mizani chini ya 18. Mtindo huu umejidhihirisha katika diwani ya *Tuzo ya Ebrahim Hussein* ukurasa wa 142 kwenye shairi la *Alipo Sikutaraji* katika ubeti pili anasema;

“Awezaye awasili, asijefanya drama,
Ajipange kwelikweli, mana jaazi lazama,
Aifungue suyuli, tufike kwenye neema
Aje kutuliza hali.”

Katika mstari wa mwisho, mwandishi ameufanya kuwa mfupi zaidi kuliko mistari mitatu iliyo tangulia.

Mtindo wa tungo-mchoro, kwa mujibu wa Muokozi (2017), katika mtindo huu shairi hupangwa katika umbo lenye kufanana na kile kinachozungumziwa. Kwa mantiki hiyo, mada inayoongelewa katika shairi hilo huonekana machoni, licha ya kusikika masikioni. Kwa mfano, kama shairi linazungumzia Mlima Kilimanjaro, mwandishi anaweza kupanga maneno katika umbo la pembe tatu ili kudhihirisha umbo la mlima. Katika diwani ya *Tuzo ya Ebrahim Hussein,* mtindo huu unajitokeza katika shairi la Mnara ukarasa wa 154, linaonekana kama ifuatavyo;


Dhiki
Haupandiki
Umegeuka sasa ni fatiki
Unazo adha na, nyingi hilaki
Unatukutisha tabu, na mingi mikiki
Una ngazi nyingi, hatari hazikanyagiki
Udhia zinateleza, mwendo sasa hautabiriki
Umejaa jingi koya, vidaraja, hata havitazamiki
Unanuka vibaya, na pua iweje, wala haisogezeki
Ukweli sakafuye imeoza, ni mbaya, wala haitamaniki
Una vumbi laumiza, linaghasi. Na macho hayafumbuki
Unapaliza pumzi, wakohoza mapafu, hakika yanapata dhiki
Unaleta lepe nayo mahepe, usingizi mwingi, kileleini haufikiki
Unalemaza miguu, kwayo vituko na maudhi,
na huwa hainyapuki
Unanyong’onyesha mwili, pia akili na urefu wake,
katu haupunguziki
Unaumiza misuli, na mifupa inayoshikana,
na mwilini huwa, haituliziki

Mwandishi ametumia umbo la mnara kuakisi kile anachokieleza katika shairi lake la *Mnara.*

www.dyampaye.co.tz

Mtindo wa takriri, kwa mujibu wa TET (2019), "mtindo wa takriri ni ujirudiaji wa neno au silabi unaofanywa kwa makusudi maalumu". Katika mtindo huu, kuna takriri katika neno ambapo mara nyingi huwa mwanzo wa mishoro na takriri katika vina vya kati au mwisho. Takriri neno hujitokeza mara chache zaidi kuliko takriri vina kwasababu watunzi wengi hupendelea kutumia takriri vina zaidi. Katika diwani ya *Tuzo ya Ebrahim Hussein,* mtindo huu unajitokeza katika shairi la *Mavulia* kwenye beti zote ameanza na takriri ya neno "Mavulia" mfano katika ubeti wa tatu anasema;

"Mavulia yanafaa, ilo sikatai sini,
Mavulia huzagaa, pande zote duniani,
Mavulia ni kinyaa, yamalizapo thamani,
Mavulia yawa kero, wenye macho lioneni."

Mtindo wa kituo, King'ei na Kemoli (2001) wanasema kituo ni mshororo wa mwisho katika ubeti ambapo maneno yaliyotumika yanaweza kutiririshwa katika beti zote. Kwa mujibu wa TET (2019), mtindo wa kituo hutokea pale ambapo mstari wa mwisho hujirudiarudia kwa kila ubeti. Kwa ujumla mtindo huu ni pale mshororo wa mwisho unaporudiwarudiwa katika beti zote za shairi husika, bila kubadilisha au kudondosha silabi au neno katika mshororo wa kituo kwa kila ubeti. Katika diwani ya *Tuzo ya Ebrahim Hussein* ukurasa wa 102 katika shairi la *Pia Ipo* mshororo wa mwisho umerudiwa katika beti zote, mfano ubeti wa kwanza anasema;

"Ni mvivu wa kusoma, ukafeli mtihani,
Kaenda omba alama, na ukapewa gizani,
Hii pia nayo ipo, usiipambe kwa lugha."

Mtindo wa kuhoji, kwa mujibu wa TET (2019), mtindo huu hutumiwa na msanii katika kuelezea mawazo yake kwa hadhira ambapo kunakuwa na hali ya kuhoji hata kama masuala yanayoongelewa yanaeleweka. Hutumia alama ya kuuliza (…?) mwisho wa tungo katika mshororo au mishororo kadhaa katika ubeti ili kumfikirisha msomaji au msikilizaji. Ingawa mbinu hii hujitokeza zaidi katika tanzu nyingine za fasihi lakini pia katika ushairi hujidhihirisha, kwa mfano katika diwani ya *Tuzo ya Ebrahim Hussein,* mtindo huu unajitokeza katika shairi la *Nani wa Kunisikia?* Ukurasa wa 158 katika ubeti wa kwanza, anasema;

"Aghalabu kila jua, huku kwetu latokea,

www.dyampaye.co.tz

Amani imepungua, nani wa kunisikia?"

Mwandishi anamtafakarisha msomaji ili abungue bongo kuwa ni nani atakayesikiliza kilio cha mwandishi.

Mtindo wa dayolojia, kwa mujibu wa TUKI (2019), "dayolojia ni maongezi yanayofanywa na wahusika katika kazi ya sanaa aghalabu tamthiliya". Ingawa mtindo huu hutumiwa zaidi katika tamthiliya, wakati mwingine katika ushairi hutumika. TET (2019) wanaongezea kwa kusema, "Mtindo huu utaitwa mtindo mmojawapo kati ya mitindo iliyotumika katika kazi ya fasihi iwapo msanii atautumia katika utanzu mwingine tofauti na tamthiliya". Hivyo katika ushairi tunaweza kupata mtindo huu, kwa mfano katika diwani ya *Tuzo ya Ebrahim Hussein,* mtindo huu unajitokeza katika shairi la *Chaguo Langu* ukurasa wa 202 katika ubeti wa kwanza, anasema;

"**Mume**

Ningekuwa malaika, niyaepuke makosa, mi nawe tungeshibana

Ila ninahangaika, utu wangu wanitosa, kutwa ninafarakana…

**Mke**

Nanenepa kuwa nawe, mume unayenijali, japo si mkamilifu,

Nakupenda kwa mayowe, naridhika kwelikweli, uwazayo upotofu…"

Mwandishi ameonyesha maongezi ya majibizano baina ya wanandoa wawili ambao wako katika mgogoro wa kimapenzi.

Mtindo wa Utomelezi, kwa mujibu TET (2019), "utomelezi humaanisha matumizi ya tanzu au vipengele vingine ndani ya utanzu mmoja". Kwa mujibu wa dhana hiyo tanzu moja mathalani katika ushairi kunakuwepo upachikwaji wa tanzu nyingine ya fasihi au baadhi ya vipengele vya utanzu huo katika beti za shairi linaloshughulikiwa. Kwa mfano katika diwani ya *Tuzo ya Ebrahim Hussein,* utomelezi umejitokeza kwa kuonyesha matumizi ya mianzo ya hadithi (Paukwa Pakawa) katika shairi la *Nchi ya Ahadi* ukarasa 132 katika ubeti wa kwanza, anasema;

"Paukwa …! Paukwa!

Kaondokea chenjaa, na kidani cha mkaa,"

Mwandishi ametumia kipengele mianzo ya hadithi kipatikanacho katika utanzu wa hadithi.

www.dyampaye.co.tz

Mtindo wa nafsi, kwa mujibu wa TET (2019), mtindo huu "hutupatia nafasi ya mwandishi na wahusika katika kazi fulani". Kuna nafsi tatu, nazo ni nafsi ya kwanza, ya pili na ya tatu, ambapo nafsi ya kwanza hutumiwa kwa lengo la kuifanya hadhira ijihisi kuwa ni mshiriki. Nafsi ya pili, huonesha kutohusika moja kwa moja kwa mwandishi juu ya mambo yanayozungumziwa huku nafsi ya tatu hutumiwa ili kuelezea matendo au tabia ya mtu mwingine. Katika diwani ya *Tuzo ya Ebrahim Hussein,* mtindo huu unajitokeza katika shairi la *Sauti ya Jalalani* ukurasa wa 236 katika ubeti wa tatu, anasema;

"Sisi ni machokoraa, ni ukweli si dhihaka,
Sababu tunapakaa, huku zitupwapo taka,
Kutoka kwenye mitaa, wenzentu mnapotoka
Napaza sauti hii, kutokea jalalani."

Mwandishi ametumia nafsi ya kwanza wingi katika neno '**tu**napakaa' (sisi) na nafsi ya pili wingi katika neno '**m**napotoka' (ninyi).

Baada ya kuona mitindo mbalimbali iliyojitokeza katika diwani ya *Tuzo ya Ebrahim Hussein*, zifuatazo ni hoja zinazofafanua dhima ya mitindo hiyo katika utunzi wa mashairi ya Kiswahili;

Kumtofautisha mtunzi mmoja na mwingine, TET (2019) wanaeleza, "Mtindo ni jinsi msanii anavyotumia ufundi na hisia zake katika kujenga upekee wa utunzi wa kazi ya fasihi". Hivyo mtindo ndio unaoifanya kazi fulani iwe tofauti na kazi za watunzi wengine hata kama jambo linaloongelewa ni lile lile. Kwa mfano, watunzi wawili wakiwa wanuzungumzia uzuri wa Mlima Kilimanjaro, mmoja kati yao akaumba maneno yake katika umbo la pembe tatu na mwingine akayaacha katika umbo la kawaida la uandishi, moja kwa moja watakuwa wametofautiana.

Kutoa msisitizo juu ya kile kinachozungumziwa, Abedi (1954) anasema desturi iliyoenea ni kukifanya kituo kuwa kiini cha habari na kukileta mwisho wa kila ubeti bila kubadilisha maneno yake. Hivyo dhima hii hutekelezwa zaidi na mitindo ya takriri pamoja na mtindo wa kituo kutokana na shairi husika. Kwanza, urudiaji wa neno moja katika kila ubeti (takriri) kunaashiria neno lile ni la muhimu na yapaswa kuzingatiwa na hadhira. Pili, kituo kinapojitokeza katika kila ubeti ni ishara ya kwamba mada au dhana ya mshororo ule ndio lengo kuu alilokusudia mtunzi limfikie hadhira wake.

www.dyampaye.co.tz

Kuunganisha dhana kati ya mshororo mmoja na unaofuata, kwa mujibu TET (2019) maneno yanayodhihirisha matumizi ya kikufu hushikamanisha mshororo na beti. Mtindo huu unasaidia kuleta muunganiko wa kile kinachozungumziwa baina ya mshororo uliotangulia na unaofuata au kati ya beti na beti. Kwa mfano katika shairi la vipande viwili kila mshororo, neno la mwisho la utao wa mshororo wa mwisho, huanzisha ukwapi wa mshororo wa kwanza katika ubeti unaofuata ili kuleta muwala kati ya beti hizo mbili.

Kumfikirisha msomaji au msikilizaji, Senkoro (1988) anasisitiza kuwa ni jukumu la hadhira kushiriki sio katika usomaji tuli bali pia kushiriki katika kuliajiri bongo. Mtunzi hutumia kauli ambayo ina alama ya kuuliza (…?) ili awafanye hadhira wake kupata tafakuri ya kina juu ya jambo mahususi. Namna hii huweza kutokea katika tungo ambayo jambo linaloongelewa linajulikana au si suala tambuka, hivyo mtunzi anaanzisha mjadala, tafakuri au tatizo, kazi inabaki kwa hadhira kubungua bongo ili kupata jawabu.

Kudhihirisha uhusianao kati ya ushairi wa Kiswahili na tanzu nyingine za fasihi, mbali na kuwa na namna ya kipekee katika utunzi wa kazi za mashairi ya Kiswahili, wakati mwingine utanzu huu huchukua baadhi ya vipengele vya tanzu nyingine na kuingiza katika mashairi hayo (Mtindo wa utomelezi). Kwa mfano shairi linaweza kuanza na mianzo ya hadithi (Paukwa Pakawa). Hali hii inaonesha kuwa mashairi ya Kiswahili yana mwingiliano na uhusiano wa kimaathiriano na tanzu nyingine za fasihi.

Kubainisha nafasi ya mtunzi na wahusika katika utungo husika, katika mtindo wa nafsi, nafasi ya mtunzi na wahusika wake hubainishwa katika nafsi tatu. Nafsi ya kwanza, mtunzi anahusika moja kwa moja kiutendaji katika jambo linaloongelewa. Nafsi ya pili anakuwa si mtendaji wa tukio hilo bali mshuhudiaji anayezungumza na mhusika mtendaji huku nafsi ya tatu, hukaa kando ya matukio kwa kueleza anachokiona bila ya kuzungumza na wahusika, bali huongea na hadhira isiyoonekana (wasomaji). Hivyo tunaweza kutambua ni wapi alikuwa mtendaji, mshuudiaji au zaidi hayo kwa kukaa mbali zaidi.

Kwa ujumla, mitindo katika utunzi wa mashairi ya Kiswahili ni mingi na huzuka mipya kadri muda uanavyozidi kwenda, mabadiliko ya jamii pamoja na kuibuka kwa watunzi chipukizi ambao huja na ubunifu tofauti na watunzi wakongwe. Wakati mwingine mitindo huweza kuwachanganya hadhira kupata maana ya kile kinachoongelewa hasa pale mtunzi anapojaribu

www.dyampaye.co.tz

kuumba maneno yake katika umbo Fulani (tungo-mchoro). Ni muhimu watunzi kuzingatia kama mitindo watakayotumia itaeleweka na hadhira waliyoikusudia au la. Hivyo wahakikishe ubunifu wao na katika kujitofautisha na watunzi wengine wanatunza maudhui yaliyowasukuma kutunga mashairi yao.

www.dyampaye.co.tz

## MAREJELEO


Abedi, K. A. (1954) *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*. Nairobi: East African Literature Bureau.

Hussein, E. (2022) *Diwani ya Tuzo ya Ushairi ya Ebrahim Hussein*. Dar es Salaam: Tanzania Growth Trust.

King'ei, G. K. na Kemoli, A. (2001) *Taaluma ya Ushairi*. Nairobi: Fotoform Limited.

Mulokozi, M. M. (2017) *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili: Kozi za Fasihi Vyuoni na Vyuo Vikuu*. Dar es Salaam: Moccony Printing Press.

Senkoro, F.E.M.K (1982) *Fasihi*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

TET (2019) *Kiswahili Shule za Sekendori Kitabu cha Mwanafunzi Kidato cha Tano na Sita: Fasihi*. Dar es Salaam: Taasisi ya Elimu Tanzania.

TUKI (2019) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu: Toleo la 4*. Dar es Salaam: TUKI.

Wamitila, K.W. (2003) *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publishers.


www.dyampaye.co.tz